HAKIMU Kneller aliye Mwakilisha Hakimu Mkuu Bw. James Wicks anaonekana akimkabidhi aliyekuwa Kadhi Mkuu wa Kenya Sheikh Farsy zawadi katika vita iliyofanyika Mombasa Islamic Centre kumwaaga baada ya kuustaafu. PICHA: NATIONAL STUDIO

Mfanyakazi bora wa Eden Rock Bw. Kahindi, Wanje (kulia) anaonekana akipokea zawadi yake kutoka kwa waziri mdogo wa nchi katika afisi ya Rais, Bw. I. K. Salat (Mwenye khanzu na kofia huko Malindi, Majuzi). PICHA: NATIONAL STUDIO.

MOMBASA YAKOSA MECHI - HAINA TAA KIWANJANI

KAMA TUNAVYOJUA kwamba Mombasa ni mji wa pili kwa ukubwa katika nchi ya Kenya. Na kwa hali yake ya kustawi sana, kibiashara na kiuchumi, na kwa vile Mji huu una banadari ya Kilindini ambayo kila siku yaingiza faida kubwa sana ya fedha, Mombasa yafikiriwa kugeuzwa na kuwa Jiji

Manispaa yenyewe ya Mombasa ambayo ina mamia ya wafanyikazi wa mshahara na mbali vibarua, inaajiri wafanyikazi wake yenyewe. Manispaa hii hii ina uwezo wa kusimamia idara ya maji ingawa wizara iliyohusika haijakubali kujitoa katika kazi hiyo na kuacha shughuli hizo ziendeshwa na Baraza la Manispaa.

Lakini kuna moja katika mji huu ambalo lahusanisha sana. Na jambo lenyewe, ni Manispaa ya Mombasa kuwa na Kiwanja cha michezo ambacho hakina mataa, jambo ambalo lingeruhusu michezo kuendelea hata usiku iwapo imelazimika kufanya hivyo. Kutokana na hali ya hewa ya Pwani, Mombasa ni mji wa joto jingi sana hasa kuanzia Disemba hadi Machi. Na lingekuwa ni jambo la maana kurakibisha ratiba za michezo ili mengine ichezwe usiku kama inavyotendeka katika miji mengine. Lakini hili lisingewezekana, kwa huu upungufu wa mataa ulioko.

Pesa za kutilia mataa kiwanja hicho zimekusanywa mara nyingi sana na watu wengi sana. Na kabla ya hapo, ni kwa nini Baraza la Manispaa liachie kazi hii watu binafsi au vyama fulani na wakati kiwanja hichi ni moja kati ya biashara zinazoletea pato Manispaa. Kiwanja cha michezo ni mtaji wa Manispaa. Cho chote kinachotendela juu ya kiwanja hicho, huwa hakitendeki bure. Kila mchezo unaochezwa hapo, Manispaa hupata fungu lake. Na mara nyengine huitwa timu kutoka nchi za jirani zicheze mechi hapa Mombasa ili pato lake lisaidie kutia Mataa uwanja huu. Jee tukiuliza pesa hizo zote zimekwendea wapi? na iwapo pesa hizo hazijatosha bado, jee mfuko huo umetengwa mbali na hesabu yake kudhibitiwa, au kwa vile pesa huwa hazitoshi na kwa hivyo ni bora zitumiwe au ziliwe kabisa?

Wakaazi wa Mombasa hawana raha kuona uwanja huu uko kizani hadi leo. Na wakaazi wazidi kutahayari wakati panapokuwa na michezo ya kujumuisha mikoa au manispaa mbali mbali na watangazaji wakaanza kuuliza, "Ziwapi taa, uwanja huu hauna taa mapka leo". Bila shaka ni dosari kubwa kwa mji kama wa Mombasa kuwa na kiwanja cha michezo ambacho hakina mataa. Na hasa pale unapoona kwamba kuna miji midogo chini ya Mombasa ambayo iko na viwanja vya michezo vyenye mataa.

Iwapo Baraza la Manispaa limeshindwa myaka yote hiyo kuwatimizia wakaazi wake ndoto yao ya kuona michezo ikiendelea katika kiwanja hicho bila ya kutishiwa na kiza, kwa nini wanasiasa hawaliingilii jambo hili.

Heko Hudaa Muslim School

NAMSHUKURU mola, kuwa, moja katika Madrasa za Mombasa, Madrasatul Hudaa wameweka mfano mwema na kianzilisho kizuri, kwa kuweka. Siku ya wazazi na kuwapa matokea ya mtihani.

Hii ni dalili ya kuwa, kweli waalimu wamawafunza wanafunzi, na Maalim Mkuu, Bw. Omar Islam, alituhakikishia kuwa ameshanzisha, madarasa yaani kutoka cha kwanza hadi cha sita.

Kwa hivyo ni wajibu wangu kumpa pongezi Bw. Omar kwa nidhamu aloiweka na bilashaka huu ni mfano mwema.

Na ni wajibu ya waalimu wa Mombasa nyingine wajaribu kuuiga, na kuzidi kuupanga uzuri, ili kwamba, nidhamu hiyo ifuatwe na vyuo vyote, na iwe si taabu, kijana anapobadilisha madrasa, kuweza kuendelea na masomo yake.

Ili kwamba mtihani mkuu wa kuigilia chuo cha pili (kinachoendelea kujengwa hivi sasa) uwe ni mmoja kwa wanafunzi wa madrasa zote, sio tu, Mombasa. Bali hata Kenya nzima.

Namuomba mola atuonyeshe haki ili tuifuate na atuoyeshe batili ili tuiepeke. Ammin.

Mohammed Ali Qoyyan.
MOMBASA.

WAISLAMU wa Afrika Mashariki kwa ujumla na khususan wale wa nchi ya Kenya wamekuwa katika heka heka za kumuaga Kadhi Mkuu wa Kenya Sheikh Abdalla Saleh El Farsy ambaye amestaafu na anaelekea kwao Oman ili apate kuishi pamoja na jamaa zake.

Hivi majuzi, huko Malindi na Lamu, kulikuwa na karamu za kumuaga chanjari ambazo ziliandaliwa na wanafunzi pamoja na wafuasi wake. Na hapa mjini Mombasa, karamu ya kumuaga Shekhe, ilifanywa Jumamosi iliyopita 23, hapo Islamic Centre munamo saa za alasiri, ambapo mamima ya Waislamu wa Mombasa na vitongoji vyake waihudhuria ili wamuage mpenzi shekhe wao. Na huo hautakuwa mwisho wa tafrija hizo, kwani pia jijini Nairobi pia angojwa afanyiwe karamu muruwa, ndipo apande ndege ya kumpeleka Maskati.

Sheikh Abdalla amekuwa Kadhi wa Kenya tokea mwaka 1967 wakati alipokuja Mombasa kutoka Zanzibar kwa minajili ya kumuagalia rafikiye mpenzi Kadhi Mkuu wa zamani Sheikh Muhamad Kassim el-Mazrui ambaye wakati huo alikuwa mgonjwa wa macho. Kwa hivyo tukiangalia tarehe ya matokeo haya, tutaona kwamba madhumuni ya sheikh kuja Mombasa, sio kutawala Ukadhi Mkuu bali ni matambezi ya kawaida ya rafikiye.

Ilipotokea yeye kupendekezwa awe Kadhi Mkuu wa Kenya, palitokea mzozo mkubwa sana na upinzani mkali toka kwa wakaazi na mashekhe wa Mombasa na wilaya nyingine. Na watu walikuwa na maoni mabali mbali ya kumpingia shekhe kuchukua wadhifa huo ambao ilikuwa ni pamoja na kuwa yeye hakuwa raia wa nchi ya Kenya.

Uraia haukuwa ni tatizo kubwa, kwani marehemu Mzee Jomo Kenyatta wakati alipokuwa Rais wa nchi hii, yeyemwenyewe alimpa uraia Sheikh Abdalla pamoja na watoto wake.

Wakati alipotawala ukadhi mkuu, Jambo kubwa Shekhe alilolilandama na akalipotezea wakati wake wote, ni Dini ya Kiislamu. Alianza kusomesha darsa katika Msikiti wa Baluchi Makadara.

Afrika Mashariki Yaondokewa na Mwanazuoni

Mara Msikiti huo ukawa mdogo kwa mujibu wa mahudhuruo ya wasikilizaji darsa hizo, na kwa hivyo akaondoka msikiti huo na akaguria Msikiti wa Shibu uliopo Mwembe Tayari.

Darasa za Farsy zilivutia watu wnegi sana. Katika mwezi mtukufu wa Ramadhan watu wakifurika katika msikiti huo kila alasiri kisikiliza darasa za Shekhe siku zote thelathini bila kuchoka.

Katika masiku ya mala mchana Shekhe pia hufanya darasa. Alianza na msikiti wa Lanfgo la Papa, kutoka hapo akenda msikiti wa Kaloleni, akaenda msikiti wa Musa, akenda Msikiti wa Sakina, akaenda Msikiti wa Neema wa King'orani.

Kutoka hapo akenda Masjidi-l-Azhar Guraya, akenda King'-orani tena huko Masjidi Ttakuwa. Na kwa hapa mjini Mombasa Msikiti wa mwisho kwenda, ni Masjidi Nnur Bondeni.

Darasa zote hizo, myaka yote hiyo, Shekhe alikuwa akizisomesha peke yake, alikuwa akizigawa siku kwa baadhi ya Msikiti, isipokuwa Azhar na Shibu, darasa za msikit hii miwilii ilikuwa hazitindiki kila wiki.

Lakini Shekhe hakumalizia darasa zake hapa Mombasa pekee bali alianza kwenda Likoni na digo yote, aghalabu siku za mwisho wa wiki. Na pia hapo sio mwisho wake kwani alikuwa pia akitembelea wilaya za Malindi na Kilifi. Na kwa hafla za Kiserikali, mara alikuwa akitembelea mji wa Nairobi na Kisumu.

Wakati Shekhe akiaga wanafunzi wake hapa Kenya, ataondoka nchi hii wakati ameshakuwa mashuhuri sana nchini kote kwa elimu yake ambayo ni kama bahari. Wanafunzi wa shekhe Abdalla ambao wamewahi kuviona baadhi ya vitabu vyake, wengine wasema kwamba ana vitabu ambavyo vyaweza kujaza vyumba vitatu na vikajaa tele.

Na ajabu ni kwamba vitabu vyote hivyo hakuviweka kama urembo bali huvipitia. Kauli ya kuaminika, yasema kwamba Shekhe ana Mashafu ndogo ndogo zifikazo arobaini ambazo huzitumia mara kwa mara.

Mashafu hizi husitumia kwa kuisoma Quran tukufu kwa viraa vyote na kwa kuwafata makurai wote saba. Fani hii si ya kawaida kwa mashekhe wetu

Tunajaribu kwa muhtasari tu kuitoa picha ya Shekhe wakati akiwaaga watu wa Kenya, lakini gazeti hili wala jengine si kufu ya misiwadi ya maelezo na tarehe ya Shekhe katika nchi hii kwa yale mengi aliyoifanyia kubwa lao likiwa kutumikia wakati wake wote kwa kuieneza haki bila ya kumjali mtu ye yote.

Mategemeo ya shekhe yalikuwa ni mawili, Quran Tukufu na zile Suna za Mtume wetu Muhammad (SAW). Kwa silaha hii ndiyo aliweza kuziteka nyoyo za wote mustamiin wa darasa zake.

Shekhe anakwenda zake lakini wanafunzi wake wapo na sisi. Mashuhuri katika hao ni Shekh Nassor Abdulrahman ambaye kwa hivi sasa ndiye ambaye ameshikilia darasa za shekhe katika msikiti yote ambayo shekhe alikuwa akisomesha.

Na pia mafunzo ya shekhe yamo katika suduri za wanafunzi pamoja na wasikilizaji, na ni imani ya watu wengi kwamba mwangaza wa elimu ambao shekhe ameuacha, hautazimwa na kiza cha kutoka popote, bali utaendelea kuangaza katika njia za haki hivyo kwamba batili isipate kurudi na watu wazidi kuishika Dini ya Mwenyezi Mungu huku wakiandama tu yale ambayo alikuja nayo Mtume wetu Muhammed (SAW).

Tukimuaga Kadhi Mkuu wa zamani, twamkaribisha Kadhi Mkuu mpya Sheikh Nassor Mohammed Al-Nahdy. Twamtakia maisha mema katika kazi yake hiyo yenye jukumu zito ya kulinda mwenendo na haki za Waislamu katika Mkuu mpya kwa maslahi ya wislamu wote wa Kenya washirikiane na Kadhi Mkuu mpya kwa maslahi ya wislamu wote wa Kenya.

Waatasimuu bihabli Ilahi jamiia walaa tatafarrakuu.

GAVANA wa Rotary International District 920, Bw. Abel Jacquemont (kulia) hivi vyombo vya kunasia sauti kwa hospital ya Port Reitz ambayo vilipokewa na Bi. Joan Ngata (kushoto) wa hospitali hiyo. PICHA: NATIONAL STUDIO

JISHINDIE
Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza maneno



SWAHILI CROSSWORD NO. 135

JINA .....

SANDUKU LA POSTA .....

KWENDA KULIA:

1. Mjanja, mdanganyi
5. Nguzo, mojawapo ya Kiislamu
7. Neema
8. South Africa
9. Aina ya samaki wa maji ya baridi
12. Neno la msangao au kushtuka!
14. Maradhi ya ngozi
15. Fujo, matata

KWENDA CHINI:

1. Mpelelezi, mchunguzi
2. Namna ya mchezo wa kitoto
3. Alama, mpaka
4. Nazi changa
6. La asumini
9. Namna ya tunda
10. Moja, kwanza
11. Ushuru, faida apatayo mtu akopeshaye fedha.
13. Kinyume cha GK

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 134

1) Zubeda Baishe, Sanduku la Posta 87019, Mombasa.

2) Mr. Juma H. Waraka, Sanduku la Posta 80353, Mombasa.

3) Bi Jedidah Wambui, Sanduku la Posta 99751, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 134 —

KWENDA KULIA:

1. WASIWASI, 6. LADHA, 7. AUMBA, 8. KARAI, 9. AU, 11. NI, 12. SHANGAZI, 14. ZI, 15. UK, 16. ZIZI, 17. CHAA

KWENDA CHINI:

1. WARAKA, 2. SHUME, 3. WALAKINI, 4. SIDIRIA, 5. KASIRIKA, 10. USHI, 11. NAZI, 13. ZUA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LIMITED*, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa- Muhariri *COASTWEEK*, Sanduku La Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tenehe 10.2.82 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.